**HOTUBA YA KATIBU MKUU KIONGOZI MHE. BALOZI DKT. MOSES MPOGOLE KUSILUKA, KWENYE UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA SITA (06) CHA SERIKALI MTANDAO KATIKA UKUMBI WA AICC – JIJINI ARUSHA, FEBRUARI 17, 2026**

---

***Ndg. Mululi Mahendeka;*** *Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu,*

***Makatibu Wakuu wote,***

***Makatibu Tawala*** *wa Mikoa na Wilaya,*

***Dkt. Musa Kissaka;*** *Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

***Mhandisi. Benedict Ndomba;*** *Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

***Wakuu*** *wa Taasisi za Umma na Binafsi,*

***Wakuu wa Idara*** *za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali*

***Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo,*** *na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao;*

***Viongozi wa Dini,***

***Waandishi wa Habari,***

*Mabibi na Mabwana;*

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujaalia uhai na afya njema, na kutuwezesha kukutana hapa leo katika Kikao Kazi hiki cha Sita (6) cha Serikali Mtandao.

Natoa shukrani za dhati kwa uongozi wa Mkoa wa Arusha kwa ushirikiano mkubwa wa kutupokea vyema, na kuwezesha kikao kazi hiki kufanyika katika mazingira rafiki, salama na yenye utulivu.

Aidha, Napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) **Dkt. Mussa Kissaka**, Mkurugenzi Mkuu **Mhandisi Benedict Ndomba,** Menejimenti na Watumishi wote wa e-GA, kwa maandalizi mazuri ya kikao hiki muhimu. Hii ni pamoja na kuwasilisha taarifa iliyoonesha hatua kubwa zilizofikiwa katika utekelezaji wa ajenda ya Serikali Mtandao nchini.

**Ndugu Washiriki;**

Kikao kazi hiki kinachowakutanisha takribani wadau 1,000 wa Serikali Mtandao ni uthibitisho wa dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi mahiri wa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA kama nyenzo muhimu ya mageuzi ya kiutendaji katika taasisi za umma, na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kaulimbiu ya Kikao Kazi hiki, *"**Kuboresha Utendaji wa Serikali kwa Kuimarisha Utoaji wa Huduma za Umma Kupitia Mifumo Salama na Jumuishi ya Serikali Mtandao",*** ina akisi kikamilifu mwelekeo wa Serikali yetu wa kuhakikisha kuwa, huduma za umma zinakuwa bora, zinazopatikana kwa wakati, kwa uwazi, kwa usalama, urahisi, haraka na kwa gharama nafuu, kwa wananchi wakati wote na mahali popote kupitia TEHAMA. Kaulimbiu hii imeakisi utekelezaji wa lengo namba 4, katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, shabaha namba 2 ambayo inaelekeza kuwa na zaidi ya

asilimia 80 ya huduma za Serikali zinazopatikana kupitia mifumo ya Kidijitali ambayo ni salama na Jumuishi.

**Ndugu Washiriki;**

Nimefarijika kusikia mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa Serikali Mtandao, ikiwemo kuimarika kwa usimamizi wa miradi ya TEHAMA Serikalini, uendeshaji wa Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali (GOVNET), uimarishaji na usimamizi wa Vituo vya Serikali vya Kuhifadhi Data (Government Data Centres), pamoja na kuwepo kwa mifumo shirikishi inayowezesha Serikali kutekeleza majukumu yake, ikiwemo kudhibiti na kusimamia mapato yake, pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Jitihada hizi zimeiwezesha Serikali kupunguza urudufu wa mifumo, kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa baina ya taasisi za umma kupitia mifumo ya TEHAMA, na hatimaye kuongeza tija, ufanisi na uwajibikaji katika utendaji kazi wa Serikali.

Vilevile, naipongeza e-GA kupitia Kituo chake cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGOVRIDC), kwa juhudi za kuendeleza tafiti na bunifu za kidijitali, hasa katika teknolojia zinazoibukia, ambazo kwa kiasi kikubwa zimesaidia kutatua changamoto katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

**Ndugu Washiriki;**

Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa sekta binafsi katika safari ya kuijenga Serikali Mtandao. Ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi, zikiwemo benki, kampuni za mawasiliano na watoa huduma za TEHAMA, ni nguzo muhimu ya mafanikio ya mageuzi ya kidijitali. Nawapongeza wadhamini wote **44** wa Kikao Kazi hiki cha Sita kwa kuonesha uzalendo na dhamira ya dhati ya kuiunga mkono Serikali.

Niungane na Mkurugenzi Ndomba kuwatambua wadhamini wakuu **Kumi (10)** wa Kikao Kazi hiki, ambao ni; **Kampuni ya Yas Mix by Yas, SOFTNET, INFO GEAR, Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Wizara ya Habari na Mawasiliano,**

**Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Shirika la Mendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Kampuni ya Simu za Mkononi VODACOM, Bodi ya Sukari (Sugar board), na Benki ya NMB.**

**Ndugu Washiriki;**

Mafanikio ya Tanzania kutambuliwa kimataifa kupitia tuzo za Umoja wa Mataifa (UN Public Service Award), World Summit on the Information Society (WSIS), na tathmini ya Benki ya Dunia ya **GovTech Maturity Index,** ni ushahidi kuwa nchi yetu ipo katika mwelekeo sahihi wa mageuzi ya Kidijitali Serikalini. Mafanikio haya si ya e-GA pekee, bali ni ya Serikali yote na Watanzania kwa ujumla.

Hata hivyo, kama ilivyoelezwa, bado tunakabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwemo kutozingatia kikamilifu Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, uhaba wa wataalamu wa TEHAMA, pamoja na kasi kubwa ya mabadiliko ya teknolojia.

Nitumie fursa hii kuzielekeza taasisi zote za umma kuzingatia kikamilifu Sheria ya Serikali Mtandao ya mwaka 2019, Kanuni zake, Viwango na Miongozo yote ya Serikali Mtandao kwa ukamilifu wake. Kila Mkuu wa taasisi ya umma, anawajibika kuhakikisha miradi yote ya TEHAMA katika taasisi yake inazingatia takwa hili la kisheria kuanzia uanzishaji, usimamizi na uendeshaji wake.

Nafahamu kuwa, ipo miradi ya TEHAMA ya Serikali inayojengwa kwa ushirikiano na sekta binafsi, lakini hii haitoi kibali kwa miradi hiyo kukiuka sheria iliyowekwa. Wakurugenzi na Wakuu wa Idara na Vitengo vya TEHAMA Serikalini, mnafahamu taratibu nzima zinazopaswa kufuatwa, ikiwa ni pamoja na kuwasilisha andiko la mradi e-GA, kabla ya kuanzisha miradi hiyo. Nawaelekeza kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa, wale wote watakaokaidi sheria hili watachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria.

Aidha, naielekeza e-GA kuwasilisha taarifa ya miradi yote ya TEHAMA Serikalini, ambayo haikuzingatia Sheria, Kanuni na Viwango vya Serikali Mtandao ili hatua zichukuliwe kwa wahusika kwa mujibu wa sheria,kupitia Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi

wa TEHAMA Serikalini (National eGovernment Steering Committee), mimi nikiwa Mwenyekiti wake.

Vilevile, nawaelekeza Mafisa Masuuli wote nchini, kuendesha vikao vya Kamati za TEHAMA za Taasisi (Institutional ICT Steering Committees) kwa wakati na kuwasilisha taarifa ya vikao hivyo e-GA kwa kila robo mwaka, hatua ambayo itasaidia kuepuka urudufu wa miradi ya TEHAMA na kuhakikisha mifumo yote ya Serikali inakuwa shirikishi, inakuwa na uwezo wa kubadilishana taarifa na inajibu mahitaji ya Taasisi husika.

**Ndugu Washiriki;**

Nimefurahishwa kusikia kuwa maazimio ya kikao kazi cha tano cha Serikali Mtandao yatawasilishwa mbele yenu, hii inaonesha ni namna gani mnaweza kujipima na kufanya ufuatiliaji wa pamoja wa utekelezaji wake. Hongereni sana!

Nawakumbusha kuwa, kikao kazi hiki cha 6 kitumike kama jukwaa la majadiliano ya wazi, kubadilishana uzoefu, kujifunza na kuweka maazimio yatakayotekelezeka na kusaidia kuharakisha mageuzi ya kidijitali Serikalini. Nawasihi washiriki wote kutumia kikamilifu fursa ya siku hizi tatu kwa manufaa ya Taifa letu.

Kutokana na uwepo wa changamoto ya usalama wa kimtandao, matumizi ya teknolojia zinazochipukia (emerging technologies) kama vile Akili Mnemba – Artificial Intelligence (AI), nategemea mtaweza kujadili kwa kina namna ya kutumia teknolojia hizi kwa uadilifu ili kulinda maslahi, mila na desturi za taifa letu.

Aidha**,** ulinzi wa taarifa binafsi na faragha upewe kipaumbele, kwa kuhakikisha taasisi za umma zinasajiliwa na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) kama inavyoelekeza Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, ili kuunga mkono jitihada za Serikali, kujenga taswira chanya ya mwelekeo wa Serikali katika ujenzi wa Serikali ya kidijitali, na kuchangia katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050.

Kwa kumalizia, napenda tena kumshukuru Mheshimiwa **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan,** kwa uongozi wake thabiti na maono yake ya kuijenga Tanzania ya kidijitali, shindani na jumuishi.

Kwa maneno hayo machache, natamka rasmi Kikao Kazi cha Sita (6) cha Serikali Mtandao kimefunguliwa.

**Kwa pamoja tuijenge Serikali Mtandao…..**

**Kazi na utu…..**

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**